## RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI.**

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeundwa chini ya kanuni ya 106, na kufafanuliwa katika jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016 na majukumu yake yameorodheshwa katika jadweli hilo. ambayo ni kama yafuatayo:-

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia

ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

v. Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viogozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu, ikiwa ni jumla ya wiki sita, ambazo zilifanyiwa kazi kama ifuatavyo.

1. Kuanzia tarehe 29/08/2016 hadi tarehe 02/09/2016, Kamati ilifanya kazi zake Unguja, na tarehe 05/09/2016 hadi 09/09/2016, Kamati ilimalizia kazi zake kwa Upande wa Pemba kwa mzunguko wa kwanza.
2. Kuanzia tarehe 31/10/2016 hadi tarehe 11/11/2016, Kamati ilifanya kazi zake Unguja kwa mzunguko wa pili.
3. Kuanzia tarehe 16/01/2017 hadi 20/01/2016, Kamati ilifanya kazi zake Unguja, na kuanzia 23/01/2017 hadi 27/01/2017, kamati ilimaliza kazi zake kwa Upande wa Dar-es-Salaam na mkoa wa Pwani kwa mzunguko wa tatu.

Kamati katika kutekeleza kazi zake ilitembelea Idara na taasisi zilizo chini yake, na kupokea taarifa za utekelezaji, kufanya ufuatiliaji katika idara hizo, pamoja na kufanya ziara na kukagua miradi mbali mbali ya maendeleo na miradi ya wananchi.

Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Kusimamia Ofsi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni hizi zifuatazo:-

1. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
2. Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

**1.0 MUUNDO WA KAMATI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Omar Seif Abeid | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Panya Ali Abdallah | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mussa Ali Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mtumwa Suleiman Makame | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |

Aidha, kamati ilikuwa makatibu wawili ambao ni:-

i. Ndg. Maryam Rashid Ali
ii. Ndg. Kassim Tafana Kassim

## SEHEMU YA PILI
## OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:-**

- Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya
- Tume ya Uchaguzi Zanzibar
- Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.
- Idara ya Kukabiliana na Maafa
- Tume ya Ukimwi
- Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ
- Idara ya Watu wenye Ulemavu
- Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa
- Baraza la Wawakilishi
- Idara ya Huduma za Makamo wa Pili wa Rais
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi
- Idara ya Mipango Sera na Utafiti
- Ofisi kuu Pemba.

**Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti Dawa za kulevya.**

Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti Kawa za kulevya kwa mwaka wa fedha 2016/2017, imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa kazi zake kwa ufanisi mkubwa, licha ya kukabilliwa na changamoto nyingi zinazoendelea kuitatiza tume hii, ambazo kwa kiasi zimekua zikikwamisha jitihada za kukabiliana na dawa za kulevya, na kupunguza athari zake kwa watumiaji wa dawa hizo. Kamati imefanya ziara katika maeneo mbali mbali kama vile Uwanja wa ndege wa Unguja na Pemba na Bandari ya Zanzibar, lengo likiwa ni kuangalia jinsi njia hizo kuu zinavyodhibitiwa kwa uingiaji wa dawa za kulevya.

Aidha kamati ilitembelea na kukagua nyumba za kurekebisha tabia, na kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya (Sober House) kwa upande wa Unguja na Pemba, na kujionea namna nyumba hizo zinavyoendeshwa. Baadhi ya nyumba zilizotembelewa ni pamoja na Detroit, Trent, Malaika sober House kwa upande wa Unguja na Limbani na Mkoroshoni kwa upande wa Pemba, ambapo nyumba ya Limbani kwa sasa imefungwa kutokana na kutokukidhi masharti na vigezo vya Sheria vya uendeshaji wa nyumba hizo.
Kwa ujumla kamati imeridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na Tume katika vita dhidi ya dawa za kulevya, pamoja na kuwepo changamoto mbali mbali wanazokabiliana nazo.

**Changamoto zinazoikabili Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti Dawa za kulevya**

1. Ufinyu wa jengo linalotumika na Tume ya Kitaifa ya uratibu na udhibiti dawa za Kulevya, ukilinganisha na mahitaji ya nafasi kwa shughuli zinazofanywa na Tume. Kamati ilijionea jengo linalotumika kwa sasa, kuwa ni chakavu na lisilokidhi mahitaji, ambapo kuna vitengo tofauti vyenye kujibana katika chumba kimoja, ikiwa ni pamoja na kitengo cha utawala, uhasibu, na sehemu inayotumika kufanya vipimo na kutoa ushauri nasaha kwa wanaofika kwenye jengo hilo.

2. Ufinyu wa Bajeti ya Tume ambao pia hupelekea kukosekana kwa vitendea kazi hasa kwa upande wa kitengo kinachojihusisha na upimaji wa afya, kinachotumika kwa ajili ya waathirika wa dawa za kulevya na wananchi kwa ujumla.

3. Ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya utendaji kazi, ambapo kamati imeelezwa kwa upande wa Pemba Tume ina vespa moja tu, jambo ambalo ni kikwazo kikubwa hasa katika ufuatiliaji wa taarifa mbali mbali za dawa za kulevya.

4. Kutomalizika kwa kesi za wanaofanya biashara za dawa za kulevya, ambapo kamati iliarifiwa kupotea kwa ushahidi mara kadhaa kwa kubadilishwa au kuibiwa kwa vielelezo vya washtakiwa, kutokuendelea kwa kesi za wanaokamatwa na dawa za kulevya, lakini pia kesi kuchukua muda mrefu sana bila kutolewa hukumu ya kesi hizo, hali ambayo inachangiwa sana na mapungufu ya kisheria iliopo kwa sasa, ambayo pia haitoi Mamlaka ya kutosha kwa Tume kutekeleza kazi zake, kwa maana nyengine tunasema Tume kutokuwa na meno katika utekelezaji wa majukumu yake.

5. Kamati ilifanya ziara yake Uwanja wa ndege na Bandari, na kubaini kutokuwepo kwa mashine ya X-ray (Unguja na Pemba) zenye uwezo wa kuona iwapo mtu amemeza kitu kisicho cha kawaida hasa dawa za kulevya katika mwili wake, na kukosekana kwa ***(Test kit)*** ambayo inatumika kuangalia kwa kitaalamu vitu vinavyohisiwa kuwa ni madawa ya kulevya.

6. Ukosefu wa chumba cha upekuzi kwa wanaoshukiwa kuwa na dawa za kulevya, ambapo kwa upande uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume International Airport, chumba kinachotumika kwa sasa, hakina faragha pale inapotokea mtuhumiwa kutiliwa shaka juu ya swala zima linalohusiana na dawa za kulevya.

7. Kutokukaguliwa kwa mizigo inayosafirishwa nje ya nchi (cargo), katika kiwanja cha Abeid Amani Karume International Airport, kunakosababishwa na kutokufanya kazi kwa mashine ya

kupekulia mizigo (Screening Mashine) iliyopo kiwanjani hapo kwa muda mrefu. Kamati ilielezwa pia kutokuwepo kwa utaratibu wa kutumia mbwa wa kutambua iwapo kuna dawa za kulevya katika mizigo inayoingizwa nchini au inayosafirishwa kwenda nje.

8. Kukosekana kwa mawasiliano ya uhakika katika ofisi za wanaohusika na upekuzi na ukaguzi wa madawa ya kulevya katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume International Airport na viwanja vya ndege vyengine ulimwenguni, jambo ambalo linaweza kutumika kuwa ni udhaifu na mwanya wa kuingiza dawa hizo haramu.

9. Kukosa ushirikiano kutoka kwa wanajamii ambao mara nyengine huwaelewa vibaya askari wanaofika katika maeneo yao kwa ajili ya doria za kupambana na wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya, suala ambalo linarudisha nyuma jitihada za tume kwa ujumla.

**Maoni na Maagizo ya Kamati**

i. Kamati imeitaka Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kuongeza Bajeti kwa ajili ya Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya katika bajeti ya mwaka 2017/2018, ili kuipa uwezo wa kifedha wa kukabiliana na janga hili la kitaifa.

ii. Kamati imeitaka Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais kuona haja ya kuifanyia marekebisho ya msingi Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya ili kuipa uwezo na Mamlaka ya kutosha ya kuzisimamia wenyewe kesi zinazohusiana na dawa za kulevya.

iii. Kamati imeshauri kuongezwa kwa wigo wa utoaji wa elimu kuhusiana na dawa za kulevya na athari zake, kwa kutumia taasisi za kijamii zaidi, ikiwa ni pamoja na shule za msingi na Madrasa za dini ambazo kuna uwezekano mkubwa wa kila kijana kupitia, ukizingatia zaidi kuwa jamii ya kizanzibar ni jamii yenye malezi ya kidini.

iv. Kamati imeshauri utolewaji wa elimu ya kutosha katika maeneo yaliyozunguka vitongoji na mitaa iliyoathirika kwa kiasi kikubwa na dawa za kulevya, kupitia mikutano ya wazi, makongamano, na warsha mbali mbali, ili kupunguza uwezekano wa janga hilo kuongezeka kwa kasi katika maeneo mengine.

v. Kamati imeshauri kuwepo kwa mikutano ya pamoja itakayofanyika mara kwa mara baina ya watendaji wa Tume, Polisi, waendesha mashtaka, mahakimu, na maofisa wa Tume ya kuzuia na kupambana na rushwa ili kujadiliana na kujenga msimamo wa pamoja wa kupambana na hatimae kutokomeza kabisa janga hili la dawa za kulevya linaloendelea kupoteza nguvu kazi ya Taifa letu.

vi. Kamati imeshauri kuboreshwa kwa mazingira ya upekuaji wa abiria na mizigo inayoingia na kutoka kupitia bandari na viwanja vya ndege kwa unguja na pemba ili kuzuia uingiaji wa dawa hizo, kwani kamati inahofia Zanzibar isijeikawa miongoni mwa njia inayotumika sana kupitishia na kusafirishia dawa za kulevya kwenda katika mataifa mengine.

vii. Kamati imeshauri kuwepo kwa mabango yanayoelezea adhabu za makosa yanayohusiana na dawa za kulevya, katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu na njia kuu za kuingia nchini kama vile bandari na uwanja wa ndege, ili kuelezea na kutoa tahadhari kuwa kujihusisha kwa namna yoyote katika dawa za kulevya ni uhalifu.

**Tume ya Uchaguzi Zanzibar**

Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi, ikiwa ni pamoja na kuendesha chaguzi mbali mbali ndani ya Zanzibar, kwa ufanisi mkubwa licha ya kuwepo kwa baadhi ya changamoto zinazoendelea kuikabili tume hiyo. Kamati ilitembelea na kukagua Ofisi ya Tume hii na kuridhishwa na utendaji wa kazi. Aidha licha ya mafaniko yaliopo katika utendaji wa kazi za Tume, Kamati imesikitishwa sana na changamoto zilizopo katika ofisi ya Tume ya Uchaguzi.

**Changamoto zinazoikabili Tume ya Uchaguzi Zanzibar**

1. Ufinyu wa majengo ya ofisi kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Kamati ilijionea kuwa jengo linalotumika kwa sasa na Tume ya Uchaguzi linatumika na Wilaya tatu ambazo ni wilaya ya Magharibi A na B, pamoja na Wilaya Mjini, hivyo kwa ujumla jengo ni finyu mno kulinganisha na mahitaji kwa sasa. Aidha katika wilaya zote (13) za Zanzibar, ni wilaya tatu tu zenye ofisi ambazo ni pamoja na, wilaya Mjini, Kusini na Kati.

2. Usalama mdogo wa jengo la Ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar kunakopelekewa na kuwepo wazi eneo hilo sambamba na kupakana na maeneo (kiwanja) yanayomilikiwa na watu binafsi.

3. Kuchakaa kwa magari mengi yanayotumika katika shughuli za Tume, kiasi cha kuifanya Tume ya Uchaguzi Zanzibar kukodi magari wakati wa utekelezaji wa shughuli zake za uchaguzi.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati.**

i. Kamati imeiagiza Serikali kupitia Ofisi ya makamo wa pili, ihakikishe Kwamba inakuwa na afisi ya Tume ya Uchaguzi katika kila Wilaya, japo kwa majengo ya kukodi kwa kuanzia huku Serikali ikitafuta namna ya kujenga ofisi zake, ili kila Wilaya iwe na Afisi yake kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma zinazotolewa na Tume ya uchaguzi karibu na maeneo yao.

ii. Kamati imeshauri kupatiwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kiwanja kilichopo jirani na jengo la Tume kinachomilikiwa na mtu binafsi kabla hajaanza ujenzi kwa hatua za awali, lakini pia, ili kuimarisha hali ya usalama zaidi kutafutwe namna ya kujengea uzio jengo la Afisi ya Tume, kwa ajili ya usalama wa watendaji na mali zake.

iii. Kamati imeshauri pia, kutokana na ufinyu wa nafasi katika jengo linalotumika kwa sasa, Serikali ifikirie kuwapatia Tume jengo liliopo jirani karibu na ofisi za Tume ambalo halitumiki kwa sasa, ili kupata eneo la kufanyia shughuli zake kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuhifadhi vifaa vyake vya uchaguzi.

iv. Kamati imeagiza kupigwa mnada na kuuza kwa magari chakavu yanayotumika na Tume ya Uchaguzi ambayo yatagharimu fedha nyingi kukarabatiwa, na badala yake yanunuliwe magari mengine mapya japo machache kwa ajili ya kuendesha shughuli za Tume, ukizingatia umuhimu wa taasisi hii

v. Kamati imeshauri kufanyika kwa program mbali mbali ambazo ni endelevu juu ya utoaji wa elimu kwa umma, juu ya kazi, nafasi na hadhi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar, ili kufuta dhana mbaya zilizopo juu ya tume hiyo kuwa si Tume huru, inayojiendesha na yenye maamuzi yake.

**Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.**

Wakala wa Serikali wa uchapaji Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi zianazosimamiwa na Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Kwa namna ya pekee, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi mkubwa iliochukua wa kuwekeza katika Kiwanda cha uchapaji, ambapo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha pamoja na kufunga mitambo mikubwa na ya kisasa, yenye kutumia teknologia ya kisasa mfano wa mitambo hiyo ni pamoja na Folding machine, web-off set machine, four colour machine nk. Kutokana na maboresho makubwa katika kiwanda cha upigaji chapa cha Serikali, kumekuwepo na changamoto kubwa ambazo bado zinahitaji kufanyiwa kazi ili lengo la kuwepo kwake liweze kufikiwa ipasavyo.

**Changamoto zinazoikabili Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.**

1. Uhaba wa wataalamu wenye ujuzi wa kuendesha mitambo mipya na ya kisasa yenye kutumia technologia mpya kabisa iliyofungwa kiwandani, na kupelekea kuzorota kwa kiasi Fulani kufikia malengo ya utowaji wa huduma wa kiwanda hicho.

2. Uhaba wa Bajeti ya kuendeshea kiwanda yaani (Running Capital), kutokana na mitambo mikubwa na ya kisasa yenye uwezo mkubwa (heavy duty), iliyofungwa kiwandani hapo, kunahitaji mtaji mkubwa wa kukiendesha, unaokisiwa kuwa ni bilioni 1.8, tofauti na bajeti shilingi 200 ilitengwa kwa mwaka huu wa fedha, ambayo kwa ujumla haikidhi mahitaji ya kuendesha idara na Kiwanda.

3. Kuwepo kwa Ushindani wa kisoko baina ya wakala wa upigaji chapa wa serikali na makampuni ya watu Binafsi, ambayo mengi yao ni yenye umaarufu na uzoefu mkubwa katika biashara ya upigaji chapa, suala ambalo nalo pia kwa namna moja kukabiliana nalo linahitaji mikakati madhubuti na uekezaji imara katika kukitangaza kiwanda hicho ili kuweza kukabiliana na ushindani uliopo.

4. Ufinyu wa ghala linalotumika kwa sasa ambalo halikidhi mahitaji kulinganisha na malengo makubwa ya kiwanda hicho na maboresho makubwa yaliyofanyika.

5. Wananchi na Wateja wengine katika soko la uchapishaji kuwa na imani ndogo au kutoamini kabisa ubora wa huduma zitolewazo na taasisi za Serikali, na kukifanya kiwanda hichi kuwa na wakati mgumu wa kufanya kazi kwa kubadili mitazamo hasi ya wateja wengi hususan kwa upande wa Zanzibar.

6. Ucheleweshaji wa malipo ya huduma zinazotolewa na kiwanda hicho, kunakofanywa na Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali, na kupelekea kurundikana kwa madeni makubwa na hatimae

kukifanya kiwanda hicho kushindwa kumudu gharama za uendeshaji kwa ujumla jambo ambalo litaitia Serikali gharama kubwa badala ya kuingiza mapato.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati**

i. Kamati imemtaka wakala wa Serikali wa Upigaji chapa Zanzibar kuchukua wataalamu kutoka kwenye makampuni mengine, ndani na nje ya Zanzibar ili kufidia pengo la ukosefu wa wataalamu wanaohitajika kiwandani hapo, kwa kuwatengezea mazingira mazuri katika maslahi watakayoyapata na kuwapatia motisha nyengine za kiutendaji kama mikataba ya kudumu na bonus ili kuendelea kuwabakisha kiwandani hapo kwa muda mrefu zaidi.

ii. Kamati imeshauri kujengwa kwa ghala jipya la kiwanda cha upigaji chapa ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha inayoendana na ukubwa wa kiwanda hicho kwa sasa. Kamati imesisitiza pia, katika mchakato wa bajeti ijayo, ujenzi ghala hilo lipewe kipaumbele kwani kiwanda kimeshaanza kufanya kazi, hivyo suala la kuwa na ghala lenye nafasi ya kutosha ni suala lisiloepukika na ni jambo linalohitaji utekelezaji wa haraka

iii. Kamati imeshauri kufanyike kwa zoezi maalum la kukitangaza kiwanda hicho kwa umma kwa ajili ya kuongeza wateja na uelewa juu ya ubora na huduma za uchapaji wa matoleo mbali mbali zinazopatikana kwa sasa.

iv. Kamati imeagiza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kutoa toleo maalum kwa Wizara, Idara na taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, linalowataka na kuwahimiza kupeleka kazi zao zote za uchapaji katika kiwanda cha uchapaji cha Serikali, zikiambatana na malipo halisi ya kazi hizo, ili kuongeza utendaji kazi na uzalishaji kiwandani hapo, na yeyote atakaekaidi agizo hilo, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake, sambamba na taasisi zenye madeni kufanya utaratibu wa haraka kulipa madeni yao ili kiwanda kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Idara ya kukabiliana na Maafa.**

Kamati inaipongeza idara ya kukabiliana na Maafa kwa jitihada inazochukua katika kuendelea na kukabiliana na maafa ya namna tofauti yanayotokea kila kukicha katika visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha kamati imefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na idara hiyo ya kutoa elimu kwa taasisi mbali mbali na wananchi kwa ujumla.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Kukabiliana na Maafa.**

1. Ukosefu wa Ghala la kuhifadhia vifaa inavyotumika wakati yanapotokea maafa hasa kwa upande wa Pemba.

2. Ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya shughuli za idara hiyo kwa ujumla ikiwa ni pamoja na fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa ghala la maafa kwa upande wa Unguja.

3. Ukosefu wa eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya wahanga wa maafa mbali mbali ya kimazingira, kama vile mafuriko, ambapo kwa sasa mara nyingi hutumika madarasa ya skuli kuwahifadhi waathirika wa majanga pale yanapotokea.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati**

i. Kamati imeitaka wizara kuiongezea Idara bajeti ya kutosha katika bajeti ya mwaka 2017/2018, ili waweze kumalizia ujenzi unaoendelea wa ghala la Maafa lililopo Unguja, na Kuanza kwa ujenzi wa Ghala jipya kwa upande wa Pemba.

ii. Kamati imeshauri kuwepo kwa zoezi endelevu la kupokea michango ya kifedha na vifaa kutoka kwa watu na wahisani mbali mbali, ili kuweza kukabiliana na maafa kwa ufanisi zaidi badala ya kuanza kutafuta misaada hiyo wakati maafa yakishatokea, na ni vyema kukawepo na akaunti maalum ya michango ya maafa itakayotumika mara moja kabla ya kupata misaada kutoka kwa wahisani wengine.

iii. Kamati imeshauri kutafutwe kwa eneo maalum ambalo litatumika kuhifadhia wahanga wa maafa makubwa yoyote yatakayotokea badala ya kutumia madara ya Skuli na kuwakosesha wanafunzi masomo kwa kipindi husika.

**Tume ya Ukimwi.**

Kamati imeridhishwa na utendaji kazi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, juu ya utekelezaji wa majukumu yake, katika vita dhidi ya UKIMWI. Aidha kamati ilipata fursa ya kutembelea jumuiya ya watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Zanizbar, ZAPHA + na kupata uelewa juu ya jitihada, mikakati shughuli, changamoto wanazokabiliana nazo, na ushirikiano baina ZAPHA+ na Tume ya Ukimwi Zanzibar.

**Changamoto zinazoikabili Tume ya Ukimwi.**

1. Kuwepo kwa maeneo ambayo yanajihusisha na biashara za ngono bila ya udhibiti wa aina yoyote, na kwa namna moja au nyengine kurudisha nyuma jitihada za Serikali dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

2. Kuwepo kwa hali ya hofu, yaani “stigma” juu ya upatikanaji wa mipira ya kuzuia maambukizi yaani “Condoms” kwa jamii, sambamba na baadhi ya wamiliki wa maduka ya madawa kuonesha mashirikiano madogo kwa kutoweka mipira hiyo katika maduka yao.

3. Kuwepo kwa unyanyapaa kwa waathirika wa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, hali ambayo sio tu inajitokeza kwa mtu mmoja mmoja moja bali mpaka katika taasisi za Serikali.

4. Ufinyu wa bajeti inayotengwa kawa ajili ya shughuli za Tume ya Ukimwi Zanzibar, kunakosababishwa pia na kupungua kwa wahisani waliokuwa wakitoa fedha kupitia miradi mbali mbali inayohusiana na UKIMWI. Changamoto hii pia imesababisha Tume kupunguza baadhi ya shughuli zake za msingi kama utoaji wa Elimu kwa jamii, na ruzuku iliyokuwa ikitolewa kwa Jumuiya zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI kama ZAPHA+.

5. Ufinyu wa huduma za ziada kwa waathirika wa Virusi vya Ukimwi, ambao mara nyingi hupatwa na magonjwa nyemelezi na kuwakwaza kiafya kutokana na kukosa huduma za ziada.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati.**

i. Kamati imeshauri kwa wizara na Serikali kwa ujumla, kuharakishwe upatikanaji wa huduma ya Bima ya Afya kwa watumishi wake, kwani suala la Bima ya afya halitawasaidia waathirika pekee isipokuwa watumishi wote wa Umma.

ii. Kamati imeshauri Tume ya Ukimwi Zanzibar kulipa kipaumbele saula la la utoaji wa elimu na kuendelea na utoaji wa elimu na kuuhamasisha umma juu athari za virusi vya ukimwi, na wasibweteke kutokana na takwimu kuuonesha kupungua kwa maambukizi ya Ukimwi–Zanzibar.

iii. Kamati imeshauri Tume ya Ukimwi Zanzibar na Serikali kwa Ujumla kutafuta namna ya kuzipa ruzuku taasisi kama ZAPHA+ ambazo zinajihusisha na kuwasaidia waathirika wengi wa Ukimwi kama zinavyopatiwa ruzuku kwa nyumba za kurekebisha tabia (Sober House).

**Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT na Muungano.**

Kamati ilipata fursa ya na kupokea taarifa juu ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT na Muungano, kwa ujumla kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Kazi za idara na inafanya vizuri katika kuhakikisha majukumu yake yanatekelezwa ipasavyo. Katika idara hii, kamati ilijikita zaidi kwa kuangalia kwa ukaribu suala la fedha za mfuko wa jimbo, miradi ya TASAF na masuala ya Muungano.

**Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ- Dar es salaam.**

Ofisi ya uratibu wa shughuli za SMZ – Dar es Salaam ni miongoni mwa ofisi zilizopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo majukumu yake ya msingi ni kuratibu shughuli za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano katika taasisi/Wizara za SMZ na zile za Muungano na kukuza na kuimarisha mashirikiano na washirika wa maendeleo,na taasisi za kibalozi. Ofisi hii imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi licha ya kuwepo kwa baadhi ya changamoto.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ- Dar es salaam.**

1. Uchakavu wa jengo; kamati ilifanya ziara na kutembelea ofisi hii na kusikitishwa na uchakavu wa jengo ukilinganisha na hadhi ya ofisi yenyewe na sehemu lilipo ni nyeti ambayo ni maeneo ya ikulu, na kupelekea taswira mbaya ya Serikali ya Zanzibar. Miongoni mwa uchakavu huo ni pamoja na paa la jengo, mandhari yote ya nje (bustani), jengo lote lina nyufa pamoja na uchakavu wa miundombinu ya maji safi na maji machafu.

2. Ushirikishwaji mdogo kati ya ofisi ya uratibu Dar es Salaam na ofisi za Zanzibar; hii inatokana na kutokupatikana kwa taarifa juu ya ufanyikaji wa vikao ambavyo ofisi ya uratibu inapaswa kuhudhuria, vile vile ofisi inapotaka taarifa kutoka wizara au taasisi za Zanzibar juu ya kuripoti katika vikao husika huwa haziwafikii kwa wakati kutoka Makao Makuu au hazipatikani kabisa.

3. Uhaba wa fedha; ofisi imetengewa bajeti finyu kwa ajili ya kazi za kawaida lakini pia hizo chache huwa hazipatikani kwa wakati, jambo ambalo hupelekea kuathirika kwa mipango ya utekelezaji waliyojipangia.

4. Uhaba wa vitendea kazi; ofisi inakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi vya ofisi, vilivyopo ni vichache na vichakavu hivyo havikidhi mahitaji ya wafanyakazi, vifaa hivyo ni kama komputa, photocopy machine, scanner, projector pamoja na samani za ofisi.

**Ushauri na Maagizo ya kamati.**

i. Kamati imeiagiza kufanywa kwa matengenezo makubwa na ya haraka ya ukarabati mkubwa wa jengo **Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ- Dar es salaam** pamoja na mazingira yanayolizunguka jengo, kutokana na kuhofia kuhamishwa ndani ya maeneo hayo muhimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukizingatia kwamba ofisi hii ndio ofisi pekee ya SMZ kwa upande wa Tanzania bara.

ii. Kamati imeagiza kuwepo kwa sera maalum ikiwemo mikakati ya lazima itakayowafanya Viongozi wa Wizara na taasisi za Zanzibar, kuitumia vizuri kikazi, Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliyopo Dar es Salaam, ili kuwepo na ufuatiliaji na upatikanaji wa taarifa zinazokuja kuwasilishwa katika vikao mbali mbali.

iii. Kamati imeitaka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kuipatia Ofisi hii fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC) na kwa wakati muafaka, kwa kuingizwa moja kwa moja kwenye akaunti yao kinyume na inavyofanyika kwa sasa. Aidha, Ofisi ipatiwe vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa, ili wafanyakazi waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

iv. Kupatiwa Mafunzo yanayoendana na Majukumu hadhi ya Ofisi, ukizingatia matumizi ya Ofisi hii kwa Viongozi mbali mbali ikiwa ni pamoja na Mabalozi na Viongozi wakuu wa chi Nchi za nje.

**Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii- TASAF**

Kamati ya kusimamia ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa katika kazi zake pia ilipata nafasi ya kukagua miradi mbali mbali iliyotekelzwa katika awamu ya kwanza na ya pili ya TASAF (TASAF I na II) ambapo kamati imefarijika sana kuona Serikali kupitia mfuko wa Maendeleo ya jamii inawasaidia wananchi katika nyanja tofauti kama vile, maji, elimu, afya na mambo mbali mbali ya kimazingira. Miongoni mwa miradi iliyotembelewa kwa Unguja na Pemba ni pamoja na mradi wa ujenzi wa tangi la maji kizimkazi dimbani, mradi wa umwagiliaji maji katika bonde la Ndijani Muembe punda, mradi wa boti za uvuvi Kizimkazi Mkunguni kwa Unguja na upande wa Pemba ni pamoja na mradi wa kisima cha maji Wingwi, mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuia maji ya bahari Micheweni, na mradi wa ujenzi wa skuli ya maandalizi Junguni. Kamati kwa kiasi kikubwa iliridhishwa na maendeleo ya miradi hii na ilibaini baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi.

**Changamoto zinazoikabili Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii- TASAF**

1. Kuwepo kwa Ushirikiano Mdogo kutoka kwa baadhi ya Wananchi kwa kutoa taarifa zisizo za kweli wanapofanyiwa mahojiano na watendaji wa TASAF, na hatimae kujikosesha haki zao katika Mradi wa Kunusuru Kaya Masikini, na kutoa nafasi kwa watu wasiostahili kupata fursa hiyo.

2. Kutofanya vizuri au kufa kabisa kwa miradi mingi iliyokwisha kamilishwa na TASAF I, na TASAF II, mara baada ya kukabidhiwa kwa Wizara husika kutakana na kukosekana kwa ufuatiliaji ulio endelevu wa taasisi husika mara baada ya TASAF kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo na kukabidhiwa kwa taasisi hizo za Serikali.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati**

i. Kamati imeshauri kutolewa kwa elimu ya kutosha kwa walengwa wa miradi ya TASAF kabla ya zoezi lolote la mradi husika kuanza, ili walengwa hao wapate uelewa wa kutosha kwa mradi husika.

ii. Kamati imeagiza kufanyika upya kwa uhakiki yakinifu wa TASAF III, ili kuwabaini watu wasio na sifa walioingizwa na kunufaika na mradi huo na kuachwa wale wenye sifa, na baada ya uhakiki huo waingizwe ili na wao waweze kunufaika, kwani Kamati inaamini bado wapo watu wanaonufaika na Mradi wa Kunusuru Kaya Masikini bila ya kuwa na sifa stahiki na kuwakosesha kupata haki wale ambao wamekusudiwa.

iii. Kamati imeshauri kuwepo na utaratibu na mpango maalum wa kufanya ukaguzi kwa miradi ya TASAF I na TASAF II, iliyokamilika na kukabidhiwa kwa sekta husika, ili miradi hiyo isiwe imetelekezwa na kukosa kufanyiwa hata matengenezo madogo pale inapotokea kuwa na hitilafu, aidha kamati inazitaka Wizara husika zinapokabidhiwa miradi ya TASAF waitunze miradi hiyo na waiendeleze miradi hiyo kwa faida ya wananchi wetu.

**Idara ya Watu Wenye Ulemavu**

Kwa ujumla kamati imeridhishwa na utendaji kazi wa idara ya Watu wenye Ulemavu. Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali zinazokwamisha juhudi zao.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Watu Wenye Ulemavu**

1. Uhaba wa bajeti; Idara ya watu wenye ulemavu imekuwa ikikabiliwa na tatizo la fedha za kutosha kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo wanashindwa kutekeleza shughuli zao kama walivyojipangia.

2. Uhaba wa vyombo vya usafiri; idara pia imekuwa na tatizo la kuwa na vyombo vya usafiri kwa ajili ya kazi zao za kila siku ukizingatia kwamba shughuli za idara hii zinahitaji ufuatiliaji wa mara kwa mara kama vile kufuatilia kesi katika mahakama mbali mbali, lakini pia kuwafuatilia waathirika mbali mbali wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji. Kwa sasa Idara ina gari moja tu, ambayo inatumika na mkurugenzi, na vespa mbili ambazo kwa ujumla hazikidhi mahitaji.

3. Uhaba wa vitendea kazi; kama vile kompyuta, mashine ya fotokopi n.k kwani vilivyopo vimechakaa sana

**Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri Wizara kuipatia Idara ya Watu wenye Ulemavu bajeti itakayokidhi mahitaji na utekelezaji majukumu yake kwa ufanisi, ukizingatia idara hii ni muhimu katika kufuatilia shughuli mbali mbali zinazofanywa na watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali.

ii. Kamati imeiagiza Ofisi ya makamo wa pili wa Rais kutafuta namna ya kuwapatia usafiri japo wa gari nyengine moja kwa ajili kazi za ufuatiliaji wa kazi za kila siku sambamba na kuwapatia vitendea kazi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

iii. Kamati inashauri kuwepo na mahusiano ya karibu baina ya Idara ya watu wenye Ulemavu na Idara ya idara ya Uwezeshaji kiuchumi, kwa kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwenye masuala ya uwezeshaji ili kuwainuwa kiuchumi kupitia vikundi vyao vva ushirika.

iv. Kamati imeshauri Idara ya watu wenye Ulemavu na Serikali kwa ujumla kulititilia mkazo suala la kueka miondo mbinu rafiki itayokidhi mahitaji ya watu wenye Ulemavu katika majengo ya zamani na mapya yanayoendele kujengwa na Serikali.

**Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa.**

Idara ya sherehe na maadhimisho ya kitaifa ina jukumu la kuratibu na kusimamia sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na kusimamia shughuli za kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 idara imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kwa namna ya pekee, kamati inatoa pongezi kwa Mhe Balozi Seif Ali Iddi ambaye ndie Mwenyekiti wa kamati ya Kitaifa ya Sherehe kwa kufanikisha maadhimisho ya kutimiza miaka 53 Sherehe za Mapinduzi kwa mwaka 2016.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa.**

1. Ufinyu wa Bajeti; idara inakabiliwa na bajeti ndogo kuweza kuhudumia shughuli zake za kila siku pamoja na kuratibu shughuli za sherehe mbali mbali za kitaifa.

2. Uhaba na uchakavu wa vifaa; kamati ilipotembelea idara hii ilipata taarifa kwamba idara haina vifaa vya kutosha kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe mbali mbali, lakini pia hivyo vilivyopo ni vya zamani na vimeshachakaa sana. Mfano wa vifaa hivyo ni mashamiana, viti na meza.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati.**

i. Kamati imeagiza kutafuta namna ya kupata fedha kwa ajili ya kununua vifaa vipya na vya kisasa ambavyo vitatumika katika shughuli na Sherehe mbali mbali za kitaifa, lakini pia vitatumika kufanyia biashara ya kuwakodisha watu binafsi kwa ajili ya kuingiza mapato Serikalini.

## OFISI YA RAIS, NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI.

**Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeundwa na idara zifuatazo:-**

- Ofisi ya Faragha
- Idara ya Mawasiliano Ikulu
- Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi
- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
- Idara ya Usalama wa Serikali (GSO)
- Idara ya ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali
- Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
- Ofisi Kuu – Pemba

**Ofisi ya faragha**.

Ofisi ya faragha ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Mhe. Rais, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zake. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ofisi hii imeendelea utekelezaji wa majukumu yake na Kamati imeridhishwa na jitihada inazozichukua kuhakikisha shughuli na ahadi za Mhe. Rais, zinatekelezwa kama zilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Faragha**

1. Ufinyu wa bajeti iliyopangwa kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa nyumba za kupumzukia za Mheshimiwa Rais, ambapo jumla ya shilingi milioni 500 zilizotengwa kwa nyumba zote Unguja na Pemba, na nyumba zinazohitaji matengenezo ni takriban zote, hivyo kwa bajeti hiyo ni vigumu kuweza kumudu kutimiza lengo lililokusudiwa.

2. Kuwepo kwa athari kubwa za kumong'onyoka kwa ardhi takriban katika nyumba zote za ikulu, nazo ni nyumba ya ikulu migombani, kibweni,bwefum na mkokotoni kwa Unguja na mkoani na chake chake (Tibirinzi ) kwa Pemba.

3. Uchakavu wa nyumba ya mapumziko ya Mhe. Rais iliyopo Laibon jijini Dar es Salaam; kamati ilitembelea nyumba hiyo na kwa kweli kamati ilisikitishwa sana na hali ya nyumba ile kuwa ni nyumba pekee anayofikia Rais wa Zanzibar, kwani ipo katika hali isiyoridhisha kabisa na haina hadhi ya kukaa kiongozi wa nchi mwenye hadhi kubwa kitaifa, nyumba ni ya zamani na haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu.

4. Usalama mdogo katika nyumba za mapumziko za Mhe. Rais, hususan katika kipindi ambacho nyumba hizo huwa hazitumiki.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati**

i. Kamati imeshauri kuimarishwa kwa suala la usafi katika maeneo ya nje ya nyumba za mapumziko ya Migombani ambayo baadhi ya maeneo ya nyumba hiyo, yamebainika kuwepo kwa hali ya mazingira yasiyoridhisha, kwa hivyo, ni vyema kukawepo na usimamizi mzuri wa kudumisha usafi wa nje kwa maeneo hayo.

ii. Kamati imeshauri, kupimwa maeneo yote ya nyumba za mapumziko za Mhe. Rais, kwa ajili ya kuwekewa uzio na kupatikana kwa nyaraka za umiliki wa eneo husika kwa nyumba hizo za Serikali.

iii. Kuhusiana na suala la mmong'onyoko wa ardhi, Kamati imeshauri kuongeza kasi ya ushughulikiaji wa tatizo hilo, ukizingatia kila siku tatizo linazidi kuongezeka hasa katika Ikulu ya Mkoani ambayo tayari hatua za ujenzi na ukarabati zinaendelea. Sambamba na ukarabati huo, kamat inasisitiza hatua za upandaji miti ni muhimu kuzingatiwa katika maeneo yalioathirika na mmong'onyoko wa ardhi.

iv. Kamati imeagiza Wizara kufanya ukarabati mkubwa katika nyumba ya Rais ya laibon- Dar es Salaam, ambayo kwa sasa haina hadhi ya kukaa Mhe. Rais, na kwa kipindi ambacho ukarabati utakuwa unaendelea ni vyema ipatikane nyumba nyengine ya hadhi yake kwa ajili ya mapumziko ya Mhe. Rais.

**Idara ya Usalama wa Serikali (GSO)**

Idara ya Usalama wa Serikali ni idara muhimu katika Serikali na ndio yenye jukumu la kusimamia masuala yote ya usalama wa Serikali kwa ujumla wake, Kamati katika utekelezaji wa kazi zake imepata nafasi ya kutembelea idara hii na kuangalia utendaji wa kazi zake za kila siku. Kiujumla kamati imeridhishwa na utendaji wa idara hii licha ya kukabiliwa na changamoto kubwa na za kimsingi.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Usalama wa Serikali (GSO)**

1. Ufinyu wa bajeti; Kamati ilibaini kuwa ofisi hii bajeti yake ni finyu sana na haikidhi mahitaji ya kazi walizojipangia na kupelekea kuzorota kwa utendaji wa kazi za Ofisi, kwa mfano

wanashindwa kufanya upekuzi (vetting) kwa waajiriwa wapya wa Serikali na kusubiri hadi ofisi au idara inayotaka kufanyiwa kazi iwape pesa ndio kazi ya upekuzi wa waajiriwa ifanyike.

2. Uchakavu wa jengo, Kamati ilitembelea jengo la ofisi hii liliopo Mnazimmoja mkabala na Ikulu na ilisikitishwa sana kuona ofisi muhimu kama hii kwa Serikali na nchi kwa ujumla, kuwa katika hali mbaya, kwani ofisi ni ndogo, paa linavuja, na haina nafasi ya kutosha na ukizingatia liko katika maeneo ya Ikulu.

3. Ukosefu wa vitendea kazi, kamati ilisikitishwa kuona hata vitendea kazi vinakosekana katika idara hii na kusababisha watendaji kutokufanya kazi zao kwa ufanisi.

4. Kukosekana kwa eneo maalum na lenye usalama kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka muhimu za Idara na Serikali kwa Ujumla.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati.**

i. Kamati inaendelea kuagiza kulifanyia ukarabati mdogo jengo linalotumika kwa sasa ili liweze kuwa na hali nzuri, agizo hili limeshakua la muda mrefu bila ya kufanyiwa kazi na kuendelea kuzorotesha utendaji wa kazi wa ofisi hii muhimu jambo ambalo pia linawavunja moyo wafanyakazi wa ofisi.

ii. Kamati imeshauri wizara kuipatia idara nyenzo za msingi za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na samani za ofisi kama vile meza, viti, kompyuta n.k.

iii. Kamati imeagiza kuongezewa bajeti idara hii katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwani ni muhimu sana kwa Serikali na watumishi wake kwa ujumla.

iv. Kamati imeshauri kufanyiwa marekebisho Sheria inayohusiana na uwepo wa Idara ya Usalama wa Serikali (GSO)-Zanzibar, ambayo kimsingi ni moja ya sababu ya kuwepo kwa changamoto nyenginezo.

**Idara ya Mawasiliano Ikulu**

Idara ya Mawasiliano Ikulu ni miongoni mwa Idara zinazounda Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwa miongoni mwa majukumu yake ya msingi kumtangaza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Idara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Mawasiliano Ikulu**

1. Kukosekana kwa huduma za kimtandao kwa baadhi ya maeneo na kusababisha kuzorota na kuchelewa kurushwa vipindi kwa wakati.

2. Mabadiliko ya haraka ya Teknologia ya Habari na mawasiliano (Tehama) ukilinganisha na kiwango cha uwezo cha kukabiliana na kuendana na mabadiliko hayo kwa idara husika.

3. Kuwepo kwa upotoshwaji wa habari kwa viongozi wa kisiasa katika kuwaelezea wanachama wao na wananchi kwa ujumla kuhusu utekelezaji na mafanikio yaliopatikana kwa Serikali kutekeleza ilani ya chama cha Mapinduzi.

4. Kukosekana kwa fursa ya kutosha na muda kupitia vyombo vya habari kwa ajili ya kuandika, kuonesha na kutangaza utekelezaji wa wa sera na mipango ya Serikali, mafanikio na changamoto zilizobaki.

**Ushauri na Maagizo ya kamati.**

i. Kamati imeshauri idara kuchukua hatua za makusudi kutoa taarifa kwa umma kwa haraka kuhusiana na upotoshwaji wa ukweli kuhusiana na mambo yanayomgusa Mhe. Rais moja kwa moja, kupitia vyombo vya habari kama TV na Radio kwani kufanya hivyo kutalinda na kuonesha uwezo, hadhi na heshima aliyonayo kiongozi wa nchi.

ii. Kamati imeshauri idara kuandaa jukwaa maalum, ambalo litamkutanisha Mhe. Rais na wadau wengine wakiwemo wanaotoka katika sekta ya habari na Biashara kwa lengo la kuboresha taswira ya Mhe Rais na kumsogeza karibu zaidi na Wananchi.

iii. Kamati imeshauri idara kuanzisha mahusiano ya karibu zaidi (networking) Na vyombo mbali mbali vya habari na wizara Nyengine, kwa lengo la kuhakisha na kuleta ufanisi wa mchakato mzima wa kuitaarifu jamii juu ya mambo mbali mbali anayoyafanya Mhe. Rais.

iv. Kamati imeagiza, kutokana na mabadiliko ya teknologia, idara ielekeze nguvu zake zaidi katika kutumia njia mpya za upokeaji na utumaji wa habari (New Media) kama mitandao ya kijamii, ikiwa ni pamoja na "*facebook*", na "*Twitter*" ambazo zina watumiaji wengi hususan vijana, mawanda mapana na haihitaji gharama kubwa.

v. Kamati pia imeshauri juu ya kuboresha tovuti ya ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi, ili kuifanya iwe ni yenye kutembelewa na watumiaji wengi na yenye kwenda na wakati zaidi.

**Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora)**

Idara hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na uhusiano wa Jumuiya za kikanda na kimataifa, aidha ni kiungo kinachowaunganisha wazanzibari wanaoishi nchi za nje kujua maendeleo ya nchi yao lakini pia kusaidia katika shughuli mbali mbali za kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sekta tofauti ikiwemo elimu na afya. Kamati inapongeza juhudi za idara hii za kufanikisha kongamano la tatu la watanzania wanaoishi nje ya nchi.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora)**

Miongoni mwa changamoto kwa Idara hii ni pamoja na Ufinyu wa ofisi za kufanyia kazi, ambapo kamati ilitembelea idara hii na kujionea maeneo ya ofisi wanazofanyia kazi kuwa hazikidhi haja kulingana na kazi zao.

**Ushauri na Maagizo ya Kamati**

Kamati imeagiza kuanza kufanyiwa kazi zaidi na kutekelezwa kwa maazimio yatokanayo na makongamano yanayoendelea kufanyika kila baada ya muda kuhusiana na Wazanzibar Wanaoishi nje ya Nchi- Diaspora.

**Ofisi ya Baraza la Mapinduzi**
Kamati imepata fursa ya kutembelea ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ambayo kimsingi ina wajibu wa kuandaa vikao vya Baraza la Mapinduzi, kamati imeridhishwa na utekelezaji wa kazi katika ofisi hii na kuridhika kuona hawana tatizo la kibajeti hivyo wanaendelea kutekelza kazi zao kama walivyojipangia.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.**
Miongoni mwa changamoto kwa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ni Ukosefu wa eneo la kutosha na lenye nafasi kwa ajili ya kuhifadhia vitabu na maktaba inayokusudiwa kutengenezwa katika Ofisi za Baraza la Mapinduzi.

**Ushauri wa Kamati**
Kutokana na mabadiliko ya haraka ya ulimwengu katika masuala ya kiteknologia, Kamati imeshauri zoezi la kuanzisha maktaba katika Ofisi za Baraza la Mapinduzi liende sambamba na kuanzishwa kwa maktaba ya kielektroniki “e-library” ili kuwawezesha waheshimiwa kutumia huduma hizo katika muda na mahala popote.

**Ofisi Kuu – PEMBA**
Kamati ilipata fursa ya kutembelea ofisi hii na kujionea miradi mbali mbali ilichini ya ofisi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2016 ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kamati imeridhiwa na utendaji kazi zake**.**
**Changamoto zinazoikabili Ofisi Kuu – PEMBA**

1. Kuwepo kwa athari kubwa za kumong’onyoko kwa ardhi katika majengo ya ofisi licha ya kufanyika kwa ukarabati mkubwa katika miaka ya hivi karibuni.

2. Kukosekana kwa maegesho rasmi yaliyojengwa kwa ajili kuhifadhia magari ya viongozi wakuu.

3. Kuwepo kwa baadhi ya magari chakavu ya Serikali ambayo hayatumiki kwa muda mrefu.

**Ushauri na Magizo ya Kamati**

i. Kamati imeshauri kufanyike kwa taratibu wa kuyapiga mnada magari chakavu ya Serikali katika ofisi hii kwa kufuata utaratibu wa uuzaji wa mali za umma.

ii. Kamati imeshauri kutengwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa maegesho maalum ya kuhifadhiwa magari ya Viongozi katika Ofisi hizo.

## SEHEMU YA TATU

**HITIMISHO**
Kwa ujumla Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeweza kufanikisha jukumu lake la msingi la kuisimamia Serikali kupitia Wizara hizi mbili kwa kiasi cha kufanyia kazi maeneo yote ambayo kamati iliona ni yenye umuhimu na kupewa kipaumbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Hivyo katika kuhakikisha kunakuwepo na utendaji uliotukuka Kamati imetoa baadhi ya mapendekezo, ushauri na maagizo ambayo Kamati inaamini yakitekelezwa na kufuatwa ipasavyo yatazisaidia sana Taasisi katika kufanikisha kazi zao na hatimae kuleta maendeleo kwa wananchi ambalo ndio lengo la Serikali.

Kwa namna ya pekee kamati inashukuru kwa mashirikiano makubwa tuliyopata kutoka katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, na Ofisi ya Rais na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, mashirikiano ambayo yameiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa viongozi wote wa Ofisi zilizo chini ya Kamati kuanzia Mhe. Rais, Dkt Ali Mohammed Shein, Mhe, Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, Mawaziri wa Ofisi zote mbili,Naibu Waziri, Makatibu wakuu na manaibu katibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya katika kuwatumikia wananchi.

Mwisho Kamati inapenda kutoa shukurani kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mhe Zubeir Ali Maulid kwa ushauri, miongozo na maelekezo mbali mbali ya kuendesha kazi za Kamati kwa ufanisi mkubwa. Aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake vizuri.